# MAOMBI

## Ya Kujikuza kiroho

SEHEMU YA 2

BY DENIS & DEVIS JULIUS

**MAOMBI MAALUMU YA KUJIKUZA KIROHO**
**Sehemu ya pili**

## SILAHA ZA HAKI.

**UTANGULIZI:**

Huu ni mwendelezo wa mwongozo wa maombi maalumu ya kujikuza kiroho. Ikiwa hujapata mwongozo wa nyuma basi unaweza kuwasiliana nasi kwa namba zilizo chini ya makala hii.

Hakuna mtu aliyezaliwa duniani, akawa anakuwa tu mwenyewe hivi hivi kwa namna ya asili bila kutegemea chakula na maji, na matunzo. Vivyo hivyo na katika roho, ukiokoka, huna budi kupata chakula na maji yako, ili uweze kukua kiroho, vinginevyo utadumaa au utakufa kabisa kabisa,
Na vitu muhimu vinavyoweza kumkuza mtu ni NENO pamoja na MAOMBI,. Ndio kama chakula na maji yetu. na jambo lingine ni “ushirika” ndio kama matunzo yetu, Hii inakuja pale tunapokusanyika pamoja kutafakari, kuabudu, kuimba, kuonyana, kufundishana na kujengana.

Hivyo kwa mwongozo wa masomo mbalimbali ya biblia unaweza kutembelea website yetu www.wingulamashahidi.org, utakutana na mafundisho zaidi ya 4,000, yatakayokusaidia kujikuza kiroho. Na pia kama utapenda kufanya ushirika na sisi basi, wasiliana nasi kwa namba zilizo mwisho wa makala hii, tukuelekeze mahali husika.

Lakini leo tunaegemea, katika eneo la ki-maombi. Tukikumbuka kuwa maombi yasipoombwa ipasavyo yanaweza pelekea tusipokee kitu kile tunachotarajia. Bwana alisema, hakuna mtu atakayemwomba Baba yake mkate akampa jiwe. Maana yake ni kuwa usipoelekeza maombi katika eneo lako ukuaji kiroho, ukaelekeza katika familia na ujenzi wa nyumba yako kamwe hutakuwa kiroho, bali utapewa haja yako. Hata kama wewe ni mwombaji mzuri.

Katika chapisho hili, tunaangazia vipengele muhimu (kwa mujibu wa biblia), ambavyo tukivigusia kwenye maombi yetu, tutakuwa tumelenga shabaha, na hakika baada ya kipindi Fulani utaona Bwana akikupigisha hatua nyingine ya kumwelewa yeye katika ukomavu wote wa rohoni.

Maombi haya ni ya SAA SITA (6) Kwa wiki. Lakini ukiomba zaidi pia ni vema. Kumbuka tumeambiwa “tukeshe tukiomba”. Tafsiri yake ni kuwa tuombe kwa muda mrefu. Kwasababu ndio maombi yenye matokeo mazuri kwa mtu. Kama mkristo jijengee desturi ya kuwa mwombaji wa masafa marefu.

~Mwl Denis & Devis Julius

# SILAHA ZA HAKI.

Maombi yetu yanaegema katika Kitabu cha Waefeso 6:12-18

*Waefeso 6:12 Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. 13 Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama. 14 Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, 15 na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani;16 zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. 17 Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu; 18 kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote;*

Huyu ni askari, sasa tengeneza picha ndio wewe. Halafu umepungukiwa na silaha hizo au mojawapo ya vitu hivyo ni kibovu. Ni wazi kuwa itakuwa ngumu kusimama vitani, hivyo utahakikisha unakiweka sawa ili uwe umekamilika kwa ajili ya kupambana na adui. Na ndio maana mstari wa 13 unasema “mkiisha kuyatimiza yote, kusimama” maana yake huwezi kusimama kama hujayatimiza yote hayo.. Huwezi kusimama kiroho kupambana na shetani kama kuna hitilafu katika imani, yako, au wokovu wako n.k.

Lakini pia mstari wa mwisho kabisa wa 18 mwandishi anasema.. “*kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote*;”

Maana yake hatuna budi kutumia muda mwingi sana kuombea hayo maeneo ya kiroho. Ndio maana kaweka msisitizo huo kwasababu alijua ni muhimu sana kwa mkristo kuwa navyo.

**Mpangalio mzuri wa silaha hizo; Ni huu**

1. **Chapeo ya wokovu kichwani**
2. **Dirii ya haki kifuani**
3. **Ngano ya imani**
4. **Kweli kiunoni**
5. **Upanga wa Roho**
6. **Utayari miguuni**

# CHAPEO YA WOKOVU: (Saa 1 (dk 60))

Chapeo ni kile chuma cha kichwani ambacho askari wanakivaa ili kujilinda na mashambulizi yanayoelekezwa kwenye eneo hilo. Kichwa ni eneo nyeti sana na ndio shabaha ya maadui kwasababu wanajua wakipiga pale ni mara moja tu,wameshamuua, Tofauti na maeneo mengine, ambayo mtu anaweza kuishi hata kama viungo hivyo havipo.

Hivyo na sisi chapeo yetu ni wokovu wetu hatuna budi kuulinda, ili tusipoteze uzima wetu.

Tunaulinda kwa kumwomba Bwana mambo haya;

## 1. Tusiiache imani:

Kuicha imani kunaweza kuja kwa namna mbili:

### a) Kuupenda ulimwengu huu:

Mfano wa hawa ni Dema ambaye tunamsoma katika;

*2Timotheo 4:10 Maana Dema aliniacha, akiupenda ulimwengu huu wa sasa, akasafiri kwenda Thesalonike..*

- ✓ Hivyo omba sana, Bwana akupe nguvu ya kuyashinda mambo ya ulimwenguni. Anasa na fahari zake zote.

### b) Kwa kupokea mafundisho mengine yasiyopata na wokovu.

Mafundisho yasiyosahihi yanaweza kukupeleka mbali na wokovu, ukaiacha imani kabisa katika Kristo Yesu, ukageukia imani za wanadamu na dini za uongo. Mfano wa Hawa alikuwa Himenayo na wengine, ambao walipokea fundisho la kwamba ufufuo wa wafu tayari umeshatokea.

*ITimotheo 1:19 uwe mwenye imani na dhamiri njema, ambayo wengine wameisukumia mbali, wakaangamia kwa habari ya Imani. 20 Katika hao wamo Himenayo na Iskanda..."*

*2Timotheo 2:17 na neno lao litaenea kama donda-ndugu. Miongoni mwa hao wamo Himenayo na Fileto, 18 walioikosa ile kweli, wakisema ya kwamba kiyama imekwisha kuwapo, hata kuipindua imani ya watu kadha wa kadha.*

- ✓ Omba sana Bwana akuepushe na mafundisho potofu ya namna hii, na dini za uongo, na roho za udanganyifu zinazozuka siku hizi za mwisho kupindua

imani, omba akupe roho ya umbanuzi, usitoke katika imani ya Kristo Yesu, udumu hapo tu, maana biblia inasema siku za mwisho watawadanganya wengi yamkini hata walio wateule.

2. **<u>Akupe ujasiri wa kuukiri wokovu wako.</u>**

Ukiri wa imani yetu katika Kristo Yesu ni nguzo muhimu. Wakati mwingine tunaona haya, au tunawaogopa wanadamu kuwaambia tumeokoka. Na hiyo inapelekea kufanya mambo ambayo Bwana ameyakataza.

Kwamfano ukishindwa kuukiri wokovu wako kwa wale waliokuwa walevi wenzako. Siku wakikuletea pombe, huwezi kuwakatalia kwasababu hawajakutambua kuwa wewe sio mwenzao. Lakini ukiwa jasiri na imani, na kuwaeleza wote bila kujali mazingira, iwe ni wafanyakazi, wanafunzi, ndugu zako. Ni ulinzi tosha wa wewe kudumu kwenye imani.Shetani alitumia silaha hii kwa watu wa kale wakashindwa kumwamini Yesu kwa hofu hii, atataka kutumia na kwako pia katika eneo fulani (Yohana 9:22).

- ✓ Hivyo omba Bwana akupe ujasiri katika ukiri wa wokovu wako.

3. **<u>Akupe kuutilia maanani wokovu wako.</u>**

Wapo watu ambao wanauchukulia wokovu kama jambo la juu juu tu, kana kwamba sio kitu cha kukilinda.. Ndugu maandiko yanasema..

*Wafilipi 2:12...bali sasa zaidi sana mimi nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka*

Lakini pia biblia inasema, wale ambao wameshaijua njia ya haki kisha wakadondoka baada ya hapo, wakarudi nyuma na kuyaishi yale maisha ya kale waliyokuwa wanayaishi ni ngumu tena kuwafanya upya.

*Waebrania 6:4 Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, 5 na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo, 6 wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri. 7 Maana nchi inayoinywa mvua inayoinyeshea mara kwa mara, na kuzaa mboga zenye manufaa kwa hao ambao kwa ajili yao yalimwa, hushiriki baraka zitokazo kwa Mungu; 6.8 bali ikitoa miiba na magugu hukataliwa na kuwa karibu na laana; ambayo mwisho wake ni kuteketezwa*

- ✓ Kwahiyo kwa vifungu hivyo ni kuomba sana Bwana akupe moyo wa kuutimiza wokovu wako kwa kuogopa na kutetemeka.

# DIRII YA HAKI. (Saa 1 (dk 60))

Dirii, ni kipande cha chuma kinachovaliwa kifuani kuzuia silaha kupenya. Eneo la kifua ni eneo la pili hatarishi, na ndio lililo kubwa kwenye mwili, hivyo shabaha kumfikia askari ni vyepesi sana.

Nasi rohoni, hatuna budi kuliombea sana. Na hapo ndipo “haki” yetu inapotulinda.

Ukiokoka shetani anatabia ya kukupofusha macho usitambue HAKI yako kwa Mungu kama mwaminio.

**Hizi ni haki ulizonazo wewe kama mtoto wa Mungu;**

**Haki ya kusamehewa dhambi:** Haijalishi ulimtenda Bwana dhambi nyingi kiasi gani, fahamu kuwa ulipotubu Bwana hazikumbuki tena dhambi zako. (Warumi 3:24 wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu;).

- ✓ Omba adui asikupige kwenye eneo hili, watu wengi wanajihukumu, au wanasikia kuhukumiwa pindi tu wajaribupo kumkaribia Bwana.. unahitaji ujasiri kwa Mungu wako. Na amekupa nafasi ya kumkaribia ili akupe mahitaji yako (Waebrania 4:16).

**Haki ya kupokea:**
Marko 11: 24 Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.

- ✓ Omba Bwana akupe ujasiri wa kufahamu kuwa lolote uombalo utapokea kwasababu yeye alisema na aliahidi.

.

**Haki ya kuitwa mwana wa Mungu:** Mwana sikuzote sio kama mtumwa au yatima, au mtu-baki. Hivyo kama Mungu amekuzaa basi tayari amekupa haki ya kulindwa na yeye, kuhudumiwa na yeye, na zaidi sana kupokea urithi wake kama mwana.

- ✓ Omba Bwana akupe ujasiri kama wa mwana kwa babaye,.(Yohana 1:12, Warumi 8:17)

**Haki ya kufunga na kufungua:** Maana yake umepewa uwezo wa kuanzisha jambo lolote(lililojema), na mbingu ikatii. Hivyo omba Bwana aondoe hofu, kwamba wewe huwezi kuunda jambo la ufalme, na likafanikiwa,au huwezi kuzivunja kazi za shetani na zikalala chini.

- ✓ Omba Bwana akupe ujasiri wa kutumia mamlaka yako rohoni.

*Mathayo 18:18  Amin, nawaambieni, yo yote mtakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yo yote mtakayoyafungua duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni.*

Soma Yohana 20:22-23,

## NGAO YA IMANI:  (Saa 1 (dk 60))

Ngao humsaidia askari kuzuia silaha, zisimfikie eneo lolote la mwili wake. Na ni muhimu sana askari kuwa na ngao, tena ile iliyo kubwa. Vivyo hivyo rohoni na sisi ni lazima eneo la ulinzi liimarike, adui asipenyeze chochote kwenye mioyo yetu. Na hiyo si nyingine zaidi ya IMANI.

Ni muhimu sana kukua “kutoka imani hata imani”. Kwasababu pasipo imani haiwezekani, kustahimili majaribu, pasipo imani haiwezekani kupokea muujiza, pasipo imani haiwezekani kumpinga adui, haiwezekani kumpendeza Mungu, pasipo imani haiwezekani kuhamisha milima(majaribu), Imani ndio nguvu ya mambo yote. Ikipungua hii silaha nyingine zote haziwezi kufanya kazi. Ndio hari na motisha ya askari vitani. Mitume walimwomba Bwana waongezewe imani kwanini wewe usiombe? (Luka 17:5)

Hivyo ni kumwomba sana Mungu akuimarishe katika eneo hili rohoni.

- ✓ Omba imani ya kuhamisha milima (matatizo)
- ✓ Imani ya kutenda miujiza
- ✓ Imani ya kupokea majibu ya maombi
- ✓ Imani ya kuzingojea ahadi za Mungu

## KWELI KIUNONI(Saa 1 (dk 60))

Askari walikuwa na mkanda maalumu unaofungwa kiunoni, ambao unalishikilia vazi, na vilevile unaambatana na kifuko cha kuhifadhia silaha ( upanga), kinachoitwa alani.

Hivyo na sisi ili tuweze kuzikaza vizuri silaha zetu zote hatuna budi kuwa na KWELI rohoni. Kweli ni Neno la Mungu lililofunuliwa.  Kwamfano wakati ule Bwana akiwa nyikani akijaribiwa na ibilisi, utaona alilitumia Neno la Mungu kumjaribu Bwana, lakini halikuwa KWELI kwasababu alilielekeza pasipolipasa kwa kumwambia Bwana ajitupe chini, kwasababu Mungu atamwagizia malaika zake wamlinde.

Lakini Bwana akaona uongo, akasema tena imeandikwa *usimjaribu Bwana Mungu wako*.
Hii ni kuonyesha kuwa tunahitaji kuifahamu KWELI yote ya Neno la Mungu na sio Neno tu. Kwasababu hata hilo shetani analitumia kuthibitisha uongo wake, kama anavyofanya sasa kwa baadhi ya watu.

Na KWELI tunaipata kwa Roho Mtakatifu, anapokaa ndani yetu, aliahidi kutuongoza katika kweli yote

*Yohana 16:13 Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake*

- ✓ Hivyo omba sana, ukielekeza maombi yako katika Roho Mtakatifu akujalie kuyaelewa maandiko katika kweli yake ili uweze kumpinga mwovu.

## UPANGA WA ROHO. (Saa 1 (dk 60))

Upanga ndio Neno la Bwana. Hivyo hatuna budi kujaa Neno lake mioyoni mwetu. Ili tuwe na shuhuda za kutosha kusimama katika vipindi vyote vya majaribu ya adui. Kwasababu ukikosa Neno la Mungu moyoni mwako, umekosa nguvu za Mungu. Kwasababu hutakuwa na ujasiri wa kupambana na mwovu, kama hujawahi ona mahali ambapo Bwana alimshinda mwovu katika eneo lako hilo.

Kwahiyo katika eneo hili ni kuomba sana Bwana akupe nguvu ya kulitumia Neno lake na sio kulisoma tu.

- ✓ Omba akutie nguvu ya kulitumia katika huduma Mungu aliyoiweka ndani yako,
- ✓ Afya yako na za wenzako.
- ✓ kazi, ulifanyayo, iwe chini ya matumizi ya kanuni za Neno
- ✓ familia yako n.k.. Ili uweze kuziangusha ngome, na kuta za shetani.

Simamia mstari huu;

Waebrania 4:12 Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. 4.13 Wala hakuna kiumbe kisichokuwa wazi mbele zake, lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pake yeye aliye na mambo yetu

## UTAYARI MIGUUNI. (Saa 1 (dk 60))

Ni Vipande vya chuma ambavyo vinavaliwa kwenye miguu, kukulinda na mashambulizi ya chini. Askari akipigwa na upanga kwenye mguu, hatoweza kutembea. Na askari mwenye vazi hili huwa na uwezo wa kupita popote kumfuata adui. Kwasababu miguu yake ipo salama.

Vivyo hivyo na sisi, hatuna budi kulivaa rohoni.
Na tafsiri yake ni INJILI. Ikiwa na maana Eneo letu la kuhubiri linapaswa liliendwe. Uzito, woga, uvivu, wa kuhubiri ni kutokana na kuwa eneo hili halipo sawa.

- ✓ Omba: Bwana akuvike ujasiri, wa kushuhudia habari ya Kristo kwa makundi yote ya watu
- ✓ Omba Bwana aweke uweza katika maneno yako. Ili yawe na ushawishi wa Roho na sio akili zako.
- ✓ Omba Bwana akuongoze kwa watu wake aliowakusudia wokovu kwa wakati husika
- ✓ Omba Mungu akujalie karama zake, na ishara zake kuambatana nawe uwapo katika kuitangaza injili yake
- ✓ Omba Mungu akufungulie mlango wa kufaa, ikiwemo vitendea kazi, (mahali palipo na ulazima kutumika)
- ✓ Omba Bwana akulinde na Yule mwovu, uwapo shambani mwa Bwana.
- ✓ Lakini pia omba Bwana anyanyue watenda-kazi wenza, watakaokusaidia kusukuma gurudumu hilo la injili. Kama vile Bwana alivyowatuma wawili wawili.

Hivyo kwa kuzingatia maombi ya muda mrefu kwenye vipengele hivi vikuu, ambapo kila kimoja utaomba kwa saa moja au zaidi, basi, utakuwa umepiga hatua kubwa sana katika eneo la kiroho. Kwasababu rohoni umekamilika kama askari mkakamavu.

Bwana akubariki.

Usikose mwendelezo mwingine.

Na, Mwl Denis & Devis Julius
Nuru_ya_ Upendo
Website: www.wingulamashahidi.org
Email: info@wingulamashahidi.org
+255693036618/ +255789001312